

Bi. Joyce Msiru amepata Elimu ya Msingi katika Shule ya Msingi Boma, Ilala kuanzia mwaka 1973-1979, akaendelea na Elimu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari ya Wanawake ya Kisutu mwaka 1980-1983 zote za jijini Dar es Salaam na Elimu ya Juu ya Sekondari katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Weruweru mkoani Kilimanjaro mwaka 1984-1986.

Akajiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kusomea Shahada ya Uchumi na Uongozi (Commerce and Management) mwaka 1987-1991 na baadae kwenda kuchukua Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Biashara (MBA in Business Administration) katika Chuo cha Central England, Birmingham nchini Uingereza mwaka 2004-2005. Aidha, alifanikiwa kupata *Certified Public Accountant (CPA T)* katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), jijini Dar es Salaam mwaka 1995.

Ana uzoefu wa kikazi kwenye taaluma ya usimamizi wa fedha katika taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo National Chemical Industries (NCI) (Januari, 1991- Mei, 1996), Pesticides Manufacturers Ltd (Juni, 1996-Juni, 1999) na kuanzia Julai, 1999 alifanya kazi katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA) katika nyadhifa mbalimbali mpaka kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa mamlaka hiyo Oktoba, 2015 na kuduma katika nafasi hiyo mpaka Oktoba, 2019.

Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) Oktoba, 2019 na kudumu katika wadhifa huo mpaka Agosti, 2021, kabla kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Wizara ya Maji Agosti, 2021.